# TNMC Habari

Toleo No. 0020

TOLEO MAALUMU Mei,2025

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari


# Watahiniwa 2,858 Wa Kada Za Uuguzi Na Ukunga Wafanya Mtihani Wa Usajili Na Leseni Mei 23, 2025.

UK. 3





## Naibu Waziri Mollel; Hongera TNMC Mnafanya kazi Nzuri

UK. 10




## Chama Cha Wauguzi Tanzania (TANNA) Chapata Uongozi Mpya

UK. 4



## Baraza la Uuguzi na Ukunga Laketi kwa Kikao Cha Robo ya Tatu Jijini Dodoma

UK. 6

# "Kutoka Dawati la Mhariri Mkuu



Karibu ujisomee Jarida la Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), lililo katika mfumo wa nakala laini, linaloandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Jarida hili linatolewa kila Mwezi likiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano wenye lengo la kuhabarisha Umma jinsi Baraza linavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

Habari na matukio tuliyokuandalia katika Jarida hili ni yale yanayohusu taaluma ya Uuguzi na Ukunga na Afya kwa ujumla.

Ikumbukwe kuwa, Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 ***(The Nursing and Midwifery Act, 2010)*** ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

**Ninakutakia usomaji mwema.**
**Asante sana**

**Bi.Agnes Mtawa**
**Msajili Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania**

## TIMU YA WAHARIRI WA JARIDA

| | |
|---|---|
| Bi. Agnes Mtawa | MWENYEKITI |
| Mwakapiso Ndimmyake | MHARIRI |
| Ezekiel Nyalusi | MSANIFU JARIDA |
| Irene Chilewa | MRATIBU |
| Rose Mhando | MRATIBU |

# Watahiniwa 2,858 Wa Kada Za Uuguzi Na Ukunga Wafanya Mtihani Wa Usajili Na Lesemi Mei 23, 2025.

*Na Mwandishi Wetu*

Jumla ya watahiniwa 2,858 waliohitimu katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi wamefanya Mtihani wa sajili na leseni unaoratibiwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) katika vituo vilivyotengwa kwenye mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza.

Mtihani huo uliofanyika Ijumaa ya Mei 23, 2025, ulijumisha watahiniwa 2,858, ambapo watahiniwa ngazi ya Astashahada 92, Stashahada 2,670 na Shahada wakiwa 96.

Wakizungumzana na TNMC habari, baadhi ya watahiniwa hao wamebainisha kuwa mtihani wa usajili na leseni ni kipimo halisi kwa wanachuo walikuwa wanazingatia mafunzo kwa vitendo wodini kwa kuwa maswali mengi yaliyoulizwa yalikuwa na lengo la kupima umahiri kwenye vitendo zaidi kuliko msomo ya nadhalia darasani.

***"Unajua wanafunzi wengi ni wavivu hawataki kwenda Wodini, wanaona wakienda wodini wanatumwa sana na wale wauguzi waliopo kwenye ajira, wanawaachia majukumu yote na wao wakati hawapati chochote na katika mtihani huu kwa wale waliokuwa wakizingatia mafunzo kwa vitendo wodini hawawezi kushindwa kujibu maana umejikita kupima weledi katika eneo la Mafunzo kwa vitendo"*** Alisema Mtahiniwa Neema Elias, kutoka Chuo cha uuguzi na ukunga Mwambani.

***'Wasimamizi wa hosipitali nchini nzima tunawaomba tunapopewa majukumu ya kufanya kazi kwenye vitengo, viongozi wa hospitali wawe wanafanya rotation ili tupate uzoefu kwenye vitengo vyote ili tukutane na wagonjwa mbalimbali hii itatusaidia kujibu mtihani wa Leseni maana huku tunaulizwa maswali yanayomgusa kila aina ya mgonjwa ambaye unaweza kukutana naye ukiwa kituoni"*** Alisema Ramadhan William ambaye ni mtahiniwa kutoka kundi la watahiniwa waliopo kazini

Mtihani wa usajili na leseni hufanyika chini ya uratibu wa Baraza la Uuguzi na Ukunga ikiwa ni utelezaji wa Sheria namba moja ya Uuguzi na Ukunga kwa mujibu wa kifungu cha 15.-(1) (a) ya mwaka 2010



# Chama Cha Wauguzi Tanzania (TANNA) Wapata Uongozi Mpya

## VIONGOZI WAPYA
## CHAMA CHA WAUGUZI TANZANIA



**EZEKEL HENRY MBAO**
RAISI WA TANNA



**PENDO MARTHA JOSEPH SHAYO**
MAKAMU WA RAISI TANNA



**CHACHA GEOFREY JOHN**
KATIBU MKUU

*Na Mwandishi Wetu*

Chama cha Wauguzi Tanzania (TANNA) mnamo tarehe 11 Mei 2025 walifanya uchaguzi na kuchagua safu mpya ya uongozi wa chama hicho utakaokuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo kwa lengo la kusimamia ustawi wa taaluma na wanataaluma wa kada ya uuguzi hapa nchini .

Uchaguzi huo wa kidemokarasi ulifanyika katika Mkutano Mkuu wa chama ulioratibiwa Mkoani Iringa.

Akitangaza Matokeo hayo mwenyekiti wa Tume ya uchaguzi Bwana Fidelis Gaakuba, amemtangaza Dkt. Ezekiel Mbao, kuwa Rais baada ya kupata kura 90 kati ya kura 153 za wajumbe wateule wenye dhamana kupiga kura kwa niaba ya wanachama, Pendo Shayo amechaguliwa kuwa makamu Rais kwa kura 71 huku nafasi ya Katibu Mkuu akichaguliwa Bw. Godfrey Chacha kwa kura 121 na katibu Mkuu msaidizi wa chama ni Meshack Makojijo, aliyechaguliwa kwa kura 96.

Viongozi wengine waliopigiwa kura na kushinda ni pamoja na Mwekahazina Mkuu ambaye Bi. Emiliana Mwakanyanga




na Mhazini msaidizi akiwa Yohana Martin huku nafasi ya katibu Mwenezi ikienda kwa Prosper Protas na katibu mwenezi msaidizi akiwa ni Maria Mtweve;

Uchaguzi huo hufanyika kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho ambapo kila baada ya miaka mitatu hutakiwa kufanya uchaguzi wa viongozi wapya watakao kiongoza chama kwa kipindi cha miaka mitatu.

Hata hivyo, Mkutano Mkuu wa TANNA wa mwaka 2026 umeadhimiwa kufanyika katika jiji la Arusha.

# TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

## AINA YA MAFUNZO YA CPD NA MGAWANYO WA ALAMA

### 1 MAFUNZO AMBAYO YANAPATIKANA ENEO LA KAZI (NON-ACCREDITED CPD)

Mafunzo haya ni yale ambayo mtaaluma anayapata kila siku eneo lake la kazi na yanapangwa na wataaluma wenyewe yakilenga kuboresha hali ya utoaji wa huduma na huduma kwa ujumla. Yanachukua asilimia 50 sawa na alama 30 ambapo mtaaluma atatakiwa kupata alama 10 kwa mwaka

### 2 MAFUNZO YALIYORATIBWA NA KUPATA ITIBATHI ( ACCREDITED CPD)

Mafunzo haya yameandaliwa na wadau mbalimbali kuanzia eneo la utoaji wa huduma na wanaosimamia miradi. Yanachukua asilimia 30 sawa na alama 18 ambapo mtaaluma atatakiwa kupata alama 6 kwa mwaka

### 3 MAFUNZO YANAYOPATIKANA KWA NJIA YA MTANDAO ( ONLINE CPD)

Mafunzo haya yanatolewa kupitia mtandao – mtaalamu anatakiwa kusoma maeneo yanayoongeza umahiri katika utoaji wa huduma. Yanachukua asilimia 20 sawa na alama 12 ambapo mtaaluma atatakiwa kupata alama 4 kwa mwaka. Mtaaluma atasoma kupitia application ya WCEA ***(https://engagement.wcea.education/tnmc)*** na National e-leaning platform - ya Wizara ya Afya

**JEDWALI : MGAWANYO WA ALAMA ZA MAFUNZO (CPD AWARDING POINTS)**

| SN | AINA YA CPD | MGAWANYO WA ALAMA % | ALAMA KWA MWAKA | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2023 | 2024 | 2025 |
| 1 | NON-ACCREDITED CPD | 50% | 10 | 10 | 10 |
| 2 | ACCREDITED CPD | 30% | 6 | 6 | 6 |
| 3 | ONLINE CPD | 20% | 4 | 4 | 4 |
| | JUMLA | 100% | 20% | 20% | 20% |

*NB: Jumla ya alama za mafunzo anazotakiwa kupata mtaaluma ili kuhuisha Leseni yake ni 60 ndani ya miaka mitatu (2023 hadi 2025)*

@tnmchabari www.tnmc.go.tz 0736 00 60 60

# Baraza la Uuguzi na Ukunga Laketi kwa Kikao Cha Robo ya Tatu Jijini Dodoma



*Na Mwandishi Wetu*

Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Prof. Lilian Mselle, ameongoza kikao cha kawaida cha robo ya tatu cha Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kilichofanyika tarehe 26.05.2025 Jijini Dodoma

Kikao hicho cha kikanuni katika uendeshaji wa Baraza kimehudhuriwa na wajumbe 12 wanaounda Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini kwa uratibu wa Msajili wa Baraza akiwa ndiye katibu wa Kikao hicho ambacho kimeangazia ajenda kadhaa ikiwa ni pamoja na kupokea, kujadili utekelezaji wa majukumu ya kurugenzi na vitengo vya Baraza kwa kipindi cha robo ya tatu yaani (Januari - Machi) ya mwaka wa Fedha 2024/2025.

Agenda nyingine ni mapitio ya yatokanayo na mkutano wa robo ya pili pamoja na kujadili na kupokea taarifa za kamati sita za Baraza,

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma ya Uuguzi na Ukunga ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga hapa nchini ni bora na salama kwa jamii.





# Wauguzi Waandamizi Wafanya Mapitio Mawanda Ya Kada Ya Uuguzi Nchini



*Na Mwandishi Wetu*

Timu ya wauguzi na wakunga wandamizi na wabobezi yenye jumla ya wajumbe 30 kutoka maeneo mbalimbali nchini wamekutana kwa siku tatu Jijini Dodoma mapema mwezi Mei kwa lengo la kupitia mawanda (Scope of Practise) ya utoaji huduma kwa kada za Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Akifungua kikao hicho muhimu kilichofanyika Jijini Dodoma, Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa, amewapongeza washiriki kwa kuitikia wito, huku akiwataka kufanya maamuzi sahihi katika eneo la mawanda ya taaluma hiyo na kubainisha kuwa, lengo la kupitia mawanda hayo ni kuhakikisha yanaendana na matakwa ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga kulinganga na mabadiliko ya Sayansi na teknolojia kwa sasa.

***"Lakini wakati mwingine sisi tuliopo Baraza, unakuta Muuguzi amefanya jambo la kuokoa maisha, lakini anachukuliwa hatua kwa kosa la kutoa huduma iliyonje na mawanda yake, jambo ambalo linatafakarisha kuwa hivi kweli yale yote tunayoyasoma miaka yote ile hata hili asingeweza kufanya?"*** Alisema Msajili Mtawa

Naye Dkt. Tegemea Mwalingo, toka Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) ambaye ni miongoni mwa timu ya wataalam waliopata fursa ya kupitia mawanda hayo, amesema marekebisho yanayofanyika kuhusu majukumu ya Muuguzi na Mkunga yatakuwa na mipaka ikiwa ni pamoja na utoaji huduma iliyo bora.

Kwa upande wake Dkt. Golden Masika, ambaye ni mratibu wa zoezi hilo, amebainisha kuwa mapitio hayo, yatawasaidia waajiri, wauguzi na wakunga, watunga sera pamoja na Serikali kuzitambua vema kada hizi mbili huku Muuguzi na Mkunga akifahamu cha kufanya pamoja na maeneo anayotakiwa kufanya kazi lakini pia wataaluma watatambulika kwa ngazi zao pamoja maslahi yao yatakuwa bora alisema Dkt. Masika.

Aidha, kikao hicho kimeandaliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga kwa kushirikiana na Mfuko wa kimataifa wa Idadi ya watu (UNFPA) na kiliketi kwa siku tatu kuanzia tarehe 27 hadi 29 Mei 2025.

# Mimi tayari nime **Subscribe** unasubiri nini?




**@tnmchabari**

Muda ni Sasa! Pata taarifa, Makala na Vipindi mbalimbali kuhusu **Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)**

# Wauguzi wa Ganzi Tiba na Usingizi Wanolewa Mloganzila



*Na Mwandishi Wetu*

Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila kwa kushirikiana chama cha wauguzi wa ganzi Tiba na usingizi nchini (ATRNA) kimetoa mafunzo maalum ya ganzi salama kwa wauguzi wa usingizi na ganzi (peripheral nerve block) kutoka Hospitali za MNH-Mloganzila, Tumbi na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Upasuaji, Dkt. Godlove Mfuko, amewapongeza wataalam hao kwa kuwa na kiu ya kujifunza na kuongeza kuwa kutokana na mabadiliko ya teknolojia na kuanzishwa kwa huduma mpya za ubingwa bobezi, ni muhimu kwa wataalam wa afya kuwa na tabia kujiendeleza kitaaluma.

Dkt. Mfuko ameongeza kuwa mahitaji ya wataalam wa ganzi na usingizi ni makubwa hivyo kitendo cha kujengeana uwezo mara kwa mara kutachochea utoaji wa huduma bora kwa wagonjwa na kuziba ombwe na upungufu wao.

***"Tuendelee kuwa wabunifu, tupende kujifunza zaidi, ukiwa na ujuzi na weledi wa kutosha utaweza kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa kumhudumia mgojwa kitu kitakachokujengea uaminifu wewe binafsi na kufanya eneo unalofanyia kazi kuaminika zaidi katika kutoa huduma husika"*** amesema Dkt. Mfuko.

Kwa upande Rais wa Chama cha Wauguzi wa Usingizi na Ganzi Bw. Hellgod Sizya amesema mafunzo hayo yatasaidia kubadilishana uzoefu wa namna ya kuendelea kutoa huduma bora za ganzi salama kwa wagonjwa wanaowahudumia.

# Naibu Waziri Mollel; Hongera TNMC Mnafanya kazi Nzuri






*Na Mwandishi Wetu*

Naibu Waziri ameyasema hayo akiwa mgeni rasmi kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya wauguzi duniani iliyoadhishwa kitaifa Mjini Iringa Mei 12.2025.

***"Nimpongeze sana Msajili na Baraza kwa ujumla, hakika Baraza hili la Uuguzi na Ukunga, limekuwa Baraza linalotekeleza majukumu yake kwa usahihi sana, unaweza kuona, linapotokea jambo la ukiukwaji wa maadili kwa Muuguzi au Mkunga, Baraza limekuwa lichukua hatua kwa wakati kwa mujibu wa Sheria ili kuhakikisha kwamba wanataaluma hawa wanatoa huduma kwa kuzingatia maadili na taratibu za taaluma hii."*** Alisema Naibu Waziri



Ameongeza kuwa TNMC imekuwa tofauti na mabaraza mengine ambayo yamekuwa yakichelewesha mashauri kwa kutochukua hatua stahiki kwa wakati ili jamii ipate huduma iliyobora na salama ikiwa ndio msingi wa kuanzishwa kwa mabaraza haya ya kitaaluma.

Siku ya wauguzi Duniani huadhishwa kila mwaka ifikapo Mei 12 ikitanguliwa na kongamano la kitaaluma la siku tatu ambapo wauguzi kutoka pende zote za nchi hukutana kwa lengo la kajadili maeandeleo ya taaluma, fursa na changamoto hivyo kuboresha utoaji huduma kwa jamii.






# Camera ya TNMC Habari

*Camera yetu imeyanasa Matukio yafuatayo*



***Bi Salome Kassanga Mkufunzi wa Mafunzo (Wapili kulia) akiwa na wauguzi baada ya Mafunzo juu ya Maadili ya Kitaaluma yaliyotolewa katika Hospitali ya Mji wa Kondoa Mei, 2025***



***Wauguzi na wakunga wakipata Mafunzo ya chumba cha upasuaji yaliyofanyika Kondoa Mji kuanzia tarehe 05-18 Mei 2025, Mafunzo yalifadhiriwa na KOFIH kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma***



***Kamati ya Ukaguzi ya Baraza iliketi Mei 14. 2025 kwa kikao chake cha kawaida cha robo ya tatu***

# Muuguzi na Mkunga Arusha Abuni Kitanda Cha Roboti




*Na Mwandishi Wetu*

Muuguzi Edward Tumoi, Afisa Muuguzi kutoka Jiji la Arusha, amebuni kitanda cha roboti chenye uwezo wa kumpokea mgonjwa na kumpeleka katika eneo la kupatiwa huduma hospitalini ikiwa ni jitihada za kuboresha mazingira ya kazi kwa wauguzi na watoa huduma kwa ujumla hospitalini.

Akizungumza kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Iringa, Tumoi amezitaja faida za kitanda hicho kiitwacho **Medical Robot Bed** ni pamoja na uwezo wa kupima uzito wa mgonjwa, kurahisisha utendaji kazi kwa kupunguza athari za kiafya zinazowapata wauguzi, hususan maumivu ya mgongo yanayotokana na kazi ya kuwanyanyua wagonjwa.

***"Nimefanya utafiti kwa zaidi ya wauguzi 340 na kubaini kuwa asilimia kubwa wanakumbwa na matatizo ya mgongo, Kupitia teknolojia hii, tunaweza kurahisisha kazi za wauguzi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za afya,"*** alisema.

***"Aidha, pamoja na kitanda nimebuni mchoro wa roboti nyingine itakayokuwa na uwezo wa kukata gozi na kupeleka sehemu husika, jambo litakalosaidia kupunguza muda na nguvu zinazotumiwa na wauguzi katika kazi hiyo ya kila siku lakini pia niwatie moyo vijana wenzangu kutumia ubunifu kama njia ya kutatua changamoto za kijamii, Kama wapo waliotengeneza mashine za CT-Scan na MRI, hata sisi tuna uwezo wa kubuni vifaa vya teknolojia ya juu kwa ajili ya Watanzania, nina imani, we can."*** Aliongeza Muuguzi Tumoi

Alihitimisha kwa kusema, gharama ya kutengeneza kitanda kimoja cha roboti ni takribani shilingi milioni 16, hivyo ameiomba Serikali na wadau wengine kuunga mkono juhudi hizo kwa vitendo badala ya kuendelea kulalamika isipokuwa kutafuta suluhu au njia mbadala za kutatua matatizo ya jamii yetu.



# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki **Mwezi MEI, 2025,** baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, **Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi** AMENI.



**JINA: MWANAISHA KATULI**
**KITUO: HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI**
**MKOA: DAR ES SALAAM**



**JINA: RUKIA RASHID RAMADHANI**
**KITUO: MWANANYAMALA RRH**
**MKOA: PWANI**



**JINA: SALOME MORRIS SHIWANDA**
**MKOA:SONGWE**



**JINA: PETER CHILEGE**
**KITUO: ST THOMAS HEALTH CENTER**
**MKOA: MOROGORO**

*"Daima **Tutawakumbuka** Wapendwa **Wetu**"*

**WAWEZA KUWASILIANA NASI KWA**

**WhatsApp**

**0737 96 26 91**

Tufuatilie katika

# Mitandao yetu ya Kijamii

@tnmchabari

LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA
www.tnmc.go.tz